



#### UFANYAJI KAZI WA DAWA



Kati ya wanawake 8 kati ya 10 wanaotumia Misoprostol watakamilisha kuavya mimba bila ya kuhitaji msaada wa dawa nyinigine yeyote ile

IWAPO DAWA  
KUFANYA KAZI



Rudia kumeza dozi ya misoprostol tena au nenda hospitali kutumia manual vacuum aspiration

Kuna hatari ndogo sana ya kasoro za uzazi ikiwa mimba itaendelea kukua baada ya kutumia misoprostol.



#### JE NILIFANIKIWA KUTOA MIMBA?

Hata kama mwanamke anahisi hana mimba ni muhimu kuhakikisha mimba imetoka. Wanawake wanatakiwa wafanye vipimo vy ujauzito au ultra sound baada ya kutoa mimba kwa kutumia misoprostol wiki 3 hadi 4 baada ya kuavya mimba



#### BAADA YA KUTOA MIMBA

Baada ya kutoa mimba mwanamke ataraje kuvuja kwa damu kidogo kwa wiki moja mpaka tatu. Lakini kila mwanamke ni tofauti. baadaye mwanamke anafaa ahakikisha uavyaji wa mimba umekamilika

Wanawake wanashauriwa wasiingize kitu chochote kwenye uke, wala kufanya ngono mpaka damu iache kutoka ukeni. inakadirisha siku 2 baada ya kutoa mimba

#### Mwanamke anaweza kupata mimba mara tu baada ya kutoa mimba

Kama hataki kupata mimba kwa haraka inabidi utumie dawa za kupanga uzazi kuhakikisha hapati mimba nyiningine isiyotarajiwu



#### CONTACTS

Women Help Women

WEB: [HTTPS://WOMENHELP.ORG/](https://WOMENHELP.ORG/)


EMAIL: [INFO@WOMENHELP.ORG](mailto:INFO@WOMENHELP.ORG)

TWITTER: [@WOMENHELPORG](https://TWITTER.COM/WOMENHELPORG)

FACEBOOK: [WOMENHELPWOMENINTERNATIONAL](https://FACEBOOK.COM/WOMENHELPWOMENINTERNATIONAL)

MAMA Network: Mobilizing Activists around Medical Abortion (MAMA).

WEB: [WWW.MAMANETWORK.ORG](http://WWW.MAMANETWORK.ORG)



UAVYAJI MIMBA  
KWA KUTUMIA DAWA  
YA MISOPROSTOL



#### JE, MISOPROSTOL

NI NINI?

Ni Dawa inayotumika dunia mzima kutoa mimba na kutibu vidonda vyu tumbo. Inauzwa katika maduka ya madawa kwa majina haya: cytote, isovent, misoclear, misofem,. Katika nchi nydingi za Afrika imesajiliwa kutibu na kuzuia uvujaji wa damu nydingi pindi mwanamke anapoifungua.



## MATUMIZI YA MISOPROSTOL

Utoaji mimba ulio salama, kutibu mwanamke aliye poteza mimba. Kutibu mwanamke aliye toa mimba (kumalizia utoaji mimba usiokamiliaka). Kuzuia na kutibu utvujaji mwangi wa damu baada ya kujifungua kutibu vidonda vya tumbo (Gastric Ulcers).

### INAFANYAJE KAZI?

Misoprotol inasababisha mchakato kama ya mimba iliyoporomoka yenye. Inalainisha na kufungua mlango wa kizazi na kufanya kizazi kusukuma na kutoa ujauzito.

### NI WAKATI GANI INAWEZA KUTUMIKA KATIKA UAVYAJI MIMBA ULIO SALAMA?



Katika wiki tisa za mwanzo wa ujauzito ukhesabu kutoka siku ya kwanza ya mzunguko wa hedhi ya mwisho.



Baada ya wiki tisa za ujauzito, inashauriwa kuitumia chini ya uangalizi wa daktari.



## INATUMIKA VIPI KWENYE UTOAJI MIMBA ULIO SALAMA?



Kijumla Mwanamke anahitaji vidonge kumi na mbili vitakavyotumiwa kwa dozi ya vidonge vine (4) kila baada ya masaa matatu (3).



Weka vidonge vinne (4) vya misoprostol chini ya ulimi

Usivimeze, viache viyeyuke mpaka viishe



kwa dakika thelathini



Baada ya masaa matatu weka vidonge vingine vinne (4) chini ya ulimi

Usivimeze, viache viyeyuke mpaka viishe



kwa dakika thelathini



Baada ya masaa matatu weka vidonge vingine vine (4) chini ya ulimi

Usivimeze, viache viyeyuke mpaka viishe



### NI NINI KINACHOTARAJIWA BAAADA YA KUTUMIA HIZO DAWA?




Maumivu na kutokwa damu Zaidi kuliko inavyotaki-kana wakati wa hedhi.



Kwenye asilimia 80% ya kesi za namna hii, mimba hutoka kwenye masaa 24 ya mwanzo



Anaweza kutumia **ibuprofen au panadol** kupunguza maumivu



## MADHARA YANAYOTARAJIWA



Ndani ya masaa 24 ya mwanzo mwanamke anaweza kupata dalili zifuatazo: kichefuchefu, kutapika, kuharisha kupata homa, kuumwa na kichwa au kusikia kizunguzungu. Hizi dalili hazina madhara na zitaisha ndani ya masaa machache



### ZIPI NI DALILI ZA (MADHARA) HATARISHI?



Kuvuja kwa damu nyangi (pedi mbili au tatu kujaa kwa zaidi yaya masaa mawili au matatu zikifuatana)



Kupatwa na joto jingi mwilini ya celcius 38 au 39 kwa zaidi ya masaa 24



Maumivu makali yasiyotibika au kupunguza kwa dawa za maumivu siku chache baada ya kumeza dawa hizo



Kutokwa na uchafu unaonuka usio wa kawaida.

### NINI CHA KUFANYA YANAPOTOKEA MATATIZO?



Nenda mara moja kwenye kituo cha afya

Ikitokea dharura, mhudumu wa afya ana wajibu wa kumuhudumu mhusika kwa wakati. Matibabu ya matatizo baada ya kutumia misoprostol **ni sawa** na na matibabu ya matatizo baada ya mimba kuperomoka yenye. Siyo rahisi kuona tofafuti kati ya mimba ilio poromoka yenye na uavyaji wa mimba ikitumia misoprostol.

**Mwanamke anayehitaji huduma ya kiafya anaweza kusema** mimba imeporomoka yenye